

TANGAZO

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI WA HALMASHAURI YA MJI NEWALA ANAWATANGAZIA WANANCHI NAFASI ZA KAZI KWA AJILI YA KUENDESHA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2019

TAREHE 01/09/2019

1. NAFASI YA MUANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA (NAFASI 189)

Sifa za Mwombaji

- Awe mtumishi wa Umma
- Awe mwaminifu na muadilifu
- Asiwe Mtendaji wa Kijiji, Mtaa au Kata
- Awe na uwezo wakuwepo katika kituo cha uandikishaji kuanzia saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni

Majukumu

- Kuandikisha Wapiga Kura kwa muda wa siku 7 kuanzia tarehe 08-14/10/2019
- Kufungua kituo cha uandikishaji wa Wapiga Kura kwa wakati kuanzia saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni

Jinsi ya Kuomba

- Andika barua kwa Msimamizi wa Uchaguzi
- Ainisha Kata na Kijiji au Mtaa ulipo na Check Number yako
- Mwisho wa kupokea maombi tarehe 20/09/2019
- Ainisha nafasi unayoiomba

2. NAFASI YA MSIMAMIZI WA KITUO (NAFASI 189)

Sifa za Mwombaji

- Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne
- Awe raia wa Tanzania
- Ikiwezekana awe mkazi wa Kata atakayofanyia kazi

- Awe mwaminifu, muadilifu, mvumilivu, mwenye hekima, busara, msikivu na anayejituma
- Asiwe Mtendaji wa Kijiji, Mtaa au Kata
- Asiwe mshabiki wa chama chochote cha siasa
- Awe tayari kutoa msaada kwa Wapiga Kura wote bila upendeleo wala ubaguzi wa aina yoyote

Majukumu

- Kupokea na kutunza vifaa vya Uchaguzi
- Kuandaa na kufungua kituo cha Kupigia Kura saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi (10) jioni
- Kuhakikisha kwamba Watendaji wa Kituo wanafahamu majukumu yao
- Kutoa ushauri na maelekezo kwa Wapiga Kura pale inapohitajika
- Kuhesabu Kura
- Kuhakikisha Mawakala waliopo Kituoni wanapewa fursa ya kujaza fomu zinazohusika
- Kushughulikia malalamiko yanayojitokeza Kituoni
- Kujaza fomu za matokeo na kuzibandika baada ya kusainiwa na Mawakala katika Kituo
- Kumtangaza Mwenyekiti wa Kitongoji aliyeshinda kwenye Kituo ambacho nafasi hiyo inagombewa
- Kuwasilisha taarifa ya Uchaguzi huo kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Mtaa/Kijiji baada ya ujwazaji wa fomu za matokeo ili Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi afanye majumuisho kupata mshindi wa jumla

Jinsi ya Kuomba

- Andika barua kwa Msimamizi wa Uchaguzi
- Ainisha sehemu ulipo (Kata), uzoefu katika shughuli za Uchaguzi na nakala ya Cheti cha Kidato cha nne (4)
- Mwisho wa kupokea maombi tarehe 10/09/2019
- Ainisha nafasi unayoiomba

3. NAFASI YA MSIMAMIZI WA KITUO MSAIDIZI (NAFASI 189)

Sifa za Mwombaji

- Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne
- Awe raia wa Tanzania
- Ikiwezekana awe mkazi wa Kata atakayofanyia kazi
- Awe mwaminifu, muadilifu, mvumilivu, mwenye hekima, busara, msikivu na anayejituma
- Asiwe Mtendaji wa Kijiji, Mtaa au Kata
- Asiwe mshabiki wa chama chochote cha siasa
- Awe tayari kutoa msaada kwa Wapiga Kura wote bila upendeleo wala ubaguzi wa aina yoyote


Majukumu

- Kumsaidia Msimamizi wa Kituo
- Kwa kushirikiana na Msimamizi wa Kituo kupokea na kutunza vifaa vya Uchaguzi
- Kuandaa na kufungua kituo cha Kupigia Kura saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi (10) jioni
- Kutoa ushauri na maelekezo kwa Wapiga Kura pale inapohitajika
- Kumsaidia Msimamizi wa Kituo kuhesabu Kura
- Kushughulikia malalamiko yanayojitokeza Kituoni

Jinsi ya Kuomba

- Andika barua kwa Msimamizi wa Uchaguzi
- Ainisha sehemu ulipo (Kata), uzoefu katika shughuli za Uchaguzi na nakala ya Cheti cha Kidato cha nne (4)
- Mwisho wa kupokea maombi tarehe 10/09/2019
- Ainisha nafasi unayoiomba

Tangazo hili limetolewa na:


Andrew F. Mgaya
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA MJI NEWALA